**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI MHESHIMIWA DR GODWIN OLOYCE MOLLEL (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA AFYA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

*(Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya kanuni za Bunge toleo la mwaka 2016)*

Ofisi ya Bunge,
S. L. P 941,
**DODOMA**

Mei, 2016.

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI MHESHIMIWA DR GODWIN OLOYCE MOLLEL (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA AFYA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**

*(Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya kanuni za Bunge toleo la mwaka 2016)*

---

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na afya njema ya kuweza kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni. Nachukua nafasi hii kumshukuru Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mhe. Freeman A. Mbowe kwa kuniamini na kuniteua kusimamia jukumu hili zito kama Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Aidha, niwashukuru wananchi wa wilaya ya Siha kwa kuniamini na kunichagua kuwa mbunge wao, bila kumsahau mke wangu Elivester Godwin Mollel ,hakika naahidi kufanya kazi hii ya uwakilishi kwa moyo mkunjufu na kamwe sitawaangusha, bali naahidi uwakilishi uliotukuka.

**Mheshima spika** Serikali ya Awamu ya Tano inadai kuwa imedhamiria kuwa ya uchumi wa kati na viwanda. Azima hii inaonekana kwenye Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016-2020). Hii itawezekana tu kwa taifa lenye afya, na lenye mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani, kwaajili ya huduma za jamii kama afya bila kutegemea Wadau wa Maendeleo.

**Mheshimiwa spika:** Wakati bajeti ya Taifa imepanda kwa zaidi ya takribani Trilioni 6.5 (kutoka trilioni 22.4 ya mwaka 2015/16 hadi trilioni 29 ya mwaka 2016/17), bajeti ya Wizara ya Afya imepungua kwa bilioni 18 kwa mwaka wa fedha 2016/17. Hii inamanisha kuwa Wizara ya Afya haijapata kipaumbele, maana yake ni kwamba huduma za afya zitakuwa mbaya na hafifu kuliko katika mwaka wa fedha

unaoisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya upinzani inaitaka serikali iongeze bajeti ya Wizara ya Afya sambamba na ongezeko la bajeti ya Taifa ili angalau sekta ya afya ibakie kuwa 11.4% ya bajeti ya Taifa kama ilivyo katika mwaka unaoisha.

**Mheshimiwa Spika,** Hali ya kupungua kwa fedha za Wadau wa Maendeleo ilianza kuonekana tangu kwenye kipindi cha serikali ya awamu ya nne, na toka mwaka wa fedha wa 2015/16 mpaka 2016/17 kwenye sekta ya afya, Wadau wa Maendeleo wamepunguza pesa za kibajeti kutoka shilingi bilioni 374.6 mpaka bilioni 198.4 ikiwa ni punguzo la shilingi bilioni 179 sawa na asilimia 47%. Hii ina maana kuwa bila ya serikali kutenga fedha zake yenyewe, huduma za afya zitadorora zaidi.

**Mheshimiwa spika,** Serikali ifanye juhudi za makusudi kutenga fedha zake yenyewe ili Wadau wa Maendeleo wakiondoka taifa letu liendelee kuwa na afya kwa kuwa afya ya wananchi ni jukumu la msingi la Serikali. Kitendo cha Serikali kushindwa kutimiza jukumu lake la msingi kumepelekea kukubali masharti yanayotolewa na ambayo inakiuka maadili, mila na tamaduni za kitanzania.

## 2.0 MFUKO WA BIMA YA AFYA YA JAMII (CHF)

**Mheshimiwa Spika**, Mpango huu uliolenga kuwahudumia wananchi nchi nzima umeonyesha kusuasua sana hususani maeneo ya vijijini. Hata hivyo unakumbwa na changamoto lukuki ikiwemo kukosa usawa yaani (***uniformity***) katika uchangiaji, baadhi ya wanachama kushindwa kuendelea kuchagia, hakuna mfumo unaoeleweka wa kufanya rufaa, uhamasishaji duni na kampeni hafifu katika kutangaza mpango huu, kutokuwa na mfumo imara wa ukusanyaji taarifa za wanachama hususani maeneo ya vijijini na kukosekana kwa mawasiliano (unreliable network) kama ilivyoainishwa katika mpango wa CHF Ulioboreshwa.

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko huu kwa muda mrefu haujaweza kuleta tija iliotegemewa hasa kwenye kufikia watu wengi, taasisi zingine za tiba zimekwepa kutokana na kuwa hela hizo kwenda wilayani na

mara nyingi haziwarudii wahusika.

**Mheshimiwa spika** kumekuwa na mifuko mbalimbali ya bima ya afya ya jamii kama CHF, TIKA etc na kumekuwa na ushauri wa kuunganisha mifuko hii.

**Mheshimiwa spika** Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri tofauti kidogo,tunashauri kuwe na bima moja ya taifa yaani NHIF kwa kila mtanzania mwenye kitambulisho cha uraia,hii itafanya taifa liwe na afya na kurahisisha uendeshaji wa shughuli za afya kuwa rahisi na uwendeshaji wa kila hospitali kuwa rahisi.

**Mheshimiwa spika** najua swali litakuwa ni nani atalipia bima hiyo kwa raia wote, jibu ni rahisi sana ni kuangalia bila kuadhiri mambo mengine wala kusababisha athari kwa thamani ya hela zetu,kwa kila kodi kuwepo kodi maalumu ya bima ya afya na uadilifu wa kutosha uwepo kupeleka gawio hilo bima

**Mheshimiwa spika** moja wapo ya hospitali zilizotembelewa na Kambi Rasmi ya Upinzani ni hospitali za binafsi zinazoendeshwa kwa kutoa huduma kwa sifa inayo lingana na hospitali zetu za wilaya na za rufaa, baadhi ya hospitali hizi kwa taarifa hazipati kabisa ruzuku kutoka serikalini lakini ubora wa huduma zake kuanzia upatikanaji wa dawa, vitendanishi, vifaa tiba na huduma, ni nzuri kuliko za serikali.

**Mheshimiwa spika** ukitizama mapato ya hospitali hizo kwa kiasi kikubwa yanatokana na bima. Hivyo basi ukiwapa watanzania wote bima kwa kiasi kikubwa hospitali zetu zitapata uwezo mkubwa wa kujitegemea kwa madawa na vitendanishi na baadhi ya vifaa tiba,vivile watu wetu watapata nafasi kubwa ya kupata huduma pale wanakoona huduma ni bora na kuongeza ushindani wenye manufaa kwa mgonjwa na taifa, lakini vivile serikali kujitoa kwenye uendeshaji wa siku hadi siku wa hospitali serikali ikajikita kwenye miradi mizito zaidi ya kuboresha afya.

## *3.0 BOHARI YA DAWA (MSD)*

**Mheshimiwa Spika:** Upungufu wa madawa unaweza kuongezeka kwani Serikali imetenga shilingi bilioni 65.1 kwa ajili ya ununuzi wa

dawa, kiasi hiki kinatosha mahitaji ya nchi kwa mwezi mmoja na nusu tu. Kwa kukadiria kuwa Tanzania ina watu takribani milioni 49.8[1] wanaohitaji matibabu, kiasi kilichotengwa kinatosha kutibu watu milioni 5.6 kwa mwaka. Je, watu wengine millioni 44 wanaobaki watatibiwa na nini na wapi?

**Mheshimiwa Spika:** Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali iongeze bajeti ya madawa kutoka 11% (shilingi bilioni 65.1) mpaka angalau 50% ya mahitaji (shilingi bilioni 295.9).

**Mheshimiwa Spika :**Ili dawa na vifaa tiba visambazwe, MSD inahitaji kupewa fedha illiyoomba. Mpaka Machi 2016,MSD walikuwa wanaidai serikali shilingi bilioni 131. Serikali imetenga shilingi bilioni 108 kulipa deni la nyuma, hivyo kubakiza deni la shilingi bilioni 23. MSD waliomba kutengewa shilingi bilioni 114 kwa ajili ya ugomboaji wa mizigo bandarini (Clearance & Forwarding) na kusambaza madawa na vifaa tiba. Wametengewa shilingi bilioni 35 tu, kiasi hiki kikipungua kwa shilingi bilioni 79.

**Mheshimiwa spika** Kiasi hiki kilichotengwa kinakidhi mahitaji ya MSD kwa miezi minne tu. Je, serikali inataka dawa na vifaa tiba viozee kwenye bohari na bandarini kwa miezi mingine? Ikiwa MSD itakopa ili kujiendesha kwa mwaka mzima, basi itahitaji kukopa shilingi bilioni 79 hivyo deni lake mpaka Juni 2017 litakuwa shilingi bilioni 102. Tutakuwa tumetengeneza deni jipya tena la kilipa mwakani .

**Mheshimiwa spika:** utaona tunaenda kutengeneza deni lingine la billion 102 kwenye eneo moja tu ,bandari na usafirishaji ,Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali iongeze bajeti ya MSD angalau kulipia deni lote ambalo baki yake ni shilingi bilioni 23 na hela za usafiri na bandari bilioni 79.

**Mheshimiwa spika:** watu wanaoishi na virusi vya ukimwi walioko kwenye dawa mpaka Machi 2015, watu 670,000 walikuwa kwenye matibabu (ARV), kiasi hicho kinakadiriwa kuongezeka na kufikia watu 988,000 mpaka Julai 2017. Kiasi kilichoombwa ni shilingi bilioni 451 lakini kiasi kilichotengwa ni takribani shilingi bilioni 48 sawa na

[1] NBS (2015) inakadiria kuwa mpaka 2014 Tanzania Bara ilikuwa na watu milioni 47.4 ongezeko la watu milioni 1.2 kwa mwaka, hivyo mpaka 2016 inakadiriwa kuwa idadi ya Watanzania ni watu milioni 49.8.

11%. Kama kwa wasitani kila mtu anahitaji dola 120 kwa mwaka, basi fedha iliyotengwa inatosha kutibu watu takribani 200,000 tu. Hii ina maana kuwa hata wale waliokuwa kwenye matibabu watakosa dawa; zaidi ya watu 400,000 watakosa dawa za ARV. Hili litakuwa ni janga jiingine.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali iongeze fedha kwa ajili ya UKIMWI kutoka 11 % (shilingi bilioni 48) mpaka angalau 50% (shilingi bilioni 218).

**Mheshimiwa Spika,** timu ya Kambi Rasmi ya Upinzani ilitembelea nchi ya kenya kujua hali ya dawa kwenye hospitali zao na kujifunza uwekezajiwa viwanda vya dawa , katika ziara hiyo nchini Kenya ,pamoja na Tanzania tumejifunza kuwa viwanda vyetu ni viwanda vya umaliziaji(finishing industry)yaani tunaagiza dawa nje tunakuja kumalizia hapa.

**Mheshimiwa spika** kwasababu tunaelekea kwenye uwekezaji hili ni eneo pia muhimu kuwekeza mfano Lushoto kuna miti ya miquinini (sinchona tree), magome yake yamebeba ndani yake alkaloid quinine ambayo hutengeneza dawa ya quinine ya kutibu malaria na dawa hii ni silaha ya mwisho kutibu malaria vilevile tunaweza kuotesha mimea ya kuzalisha ambayo majani yake hutumika kwaajili ya dawa mseto marufu ALU(Artemisia) na mengine mengi ambazo zinastawi katika nchi za tropikali.

**Mheshimiwa spika** ninataja haya hapa juu kwani kwenye viwanda vyetu katika nchi mbili hizi tunaagiza malighafi inayoweza kuzalishwa hapa ili kupunguza gharama za tiba, kurahisisha upatikanaji wa dawa na kuchangia pato la taifa

## 4.0 AFYA YA MAMA NA MTOTO

**Mheshimwa Spika,** Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 46 (1) (g) kinaeleza wazi haki za wanawake kupata huduma za afya (women with the right to health care). Pamoja na haki zao kutambuliwa katika katiba na sera mbalimbali bado wanawake wamekuwa wakiteseka sana na wengi kupoteza maisha kwa sababu za huduma duni za afya. Waathirika mkubwa zaidi katika sekta hii ya afya ni wanawake wajawazito na watoto.

**Mheshimiwa Spika**, Hali ya vifo vinavyotokana na uzazi katika nchi yetu ni ya kutisha. Katika ripoti ya Bank ya Dunia mwaka huu wa 2016 (World Bank 2016 Martenal mortality ratio) takwimu zinaonyesha vifo vilivyotokana na uzazi (maternal mortality rate) kwa mwaka 2011 (483) 2012 (464) 2013 (438) 2014(418) na 2015(398) kwa kila wanawake 100,000**.** Hali hii inaonyesha bado juhudi zaidi zinaitajika kufanywa serikali kuhakikisha inapunguza kabisa vifo vya kina mama vinatokana na uzazi.

**Mheshimiwa spika** Kiwango hiki ni sawa na akina Mama 1,255 kwa mwezi na akina Mama 42 kila siku sawa na akina Mama wawili kwa saa. Kama ukiwakusanya hawa akina Mama wanaofariki, ni zaidi ya basi la abiria aina ya Costa wanakufa kila siku.

**Mheshimiwa Spika**, katika jamii zetu tunatambua mchango mkubwa anaoutoa mama katika malezi na makuzi ya familia ikiwemo kuchangia katika kipato cha familia (women contribute substantially to household income). Pamoja na hayo wanawake wanatoa mchango mkubwa sana katika kukuza uchumi wa nchi hii japo wengi hufanya kazi katika mfumo usio rasmi tena kwa kipato kidogo na mazingira magumu sana.

**Mheshimiwa Spika**, Mchango mkubwa alionao mwanamke ndani ya familia na taifa kwa ujumla ni vema serikali ikauthamini sana. Mama anapofariki mara nyingi wale waliobaki katika familia huishi kwa tabu sana familia nyingine husambaratika kabisa. Watoto wengi wameishia kuwa omba omba, kujihusisha na biashara za ngono na madawa ya kulevya na hata kukosa kabisa mwelekeo wa kimaisha. Kwa umuhimu wa kipekee serikali haina budi kuja na mkakati wenye tija wa kupunguza vifo vya kina mama husussani vinavyotokana na uzazi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuhakikisha inakuja na mpango madhubuti ulio rahisi katika utekelezaji zinaonyesha viko juu sana. Ni lazima serikali itekeleleze wajibu wake ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa mtoto na mama wanaishi kama agenda ya kitaifa (Make Child and mother survival a

core national health concern). Vilevile, **Kambi Rasmi ya Upinzani** inaitaka serikali kufanya tathimini ya uhakika kuhakikisha inajua idadi kamili ya vifo vya mama vinavyotokana na uzazi kwa kuwa bado kina mama wengi wanazalia majumbani haswa maeneo ya vijijini ili kuweza kubaini athari za kiuchumi zinazotokana na vifo vya kina mama pamoja na kupata mkakati wa kutatua tatizo. (evidence based strategies) kuhakikisha inapunguza vifo vinavyotokana na uzazi kwa kina mama ambavyo bado takwimu siyo za kutosheleza.

**Mheshimiwa Spika,** Ikumbukwe kuwa mwaka 2010/2011 bajaj 400 zilinunuliwa kwa fedha za walipa kodi ili zitumike kama 'ambulance' za kusafirisha wajawazito kwenda hospitalini. Kambi Rasmi ya Upinzani inazo taarifa za uhakika za kushindwa kufanya kazi kwa bajaj hizo na nyingi kutelekezwa kutokana na changamoto za jiografia ya maeneo mbalimbali na ubovu wa miundombinu. Haya ni matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi lakini ni dhihaka kwa wajawazito nchini

**Mheshimiwa spika** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaihoji Serikali ni kigezo gani walitumia kufikia maamuzi ya kununua pikipiki hizo ambazo ziligharimu milioni 26 kwa moja, huku ikionekana kabisa pikipiki hizo mama akikamatwa na uchungu akiwa juu ya pikipiki hiyo uwezekano wa kuipindua pikipiki hiyo ni mkubwa sana .

### 4.1 Haki jinsia na afya ya Mwanamke .

**Mheshimiwa Spika**, kuna uhusiana mkubwa sana katika kuongeza raslimali katika elimu ya mtoto wa kike na kuboresha afya ya mama , mtoto na jamii kwa ujumla ,vilevile uhusiano na kupata jamii vumbuzi **(innovative society)** ,

**Mheshimiwa spika** zifanyike jitihada za makusudi kuondoa kabisa mila na desturi zinazo puuza uwezo wa akili ya mwanamke na nafasi ya mwanamke kwenye jamii.

**Mheshimiwa Spika**, kuthamini akili ya mwanamke ,kuheshimu mwili wa mwanamke na kumpa mwanamke elimu bora siyo tu itaboresha maisha ya mwanamke bali italiboresha TAIFA

## 5.0 TATIZO LA UTAPIAMLO KWA WATOTO NCHINI

**Mheshimwa Spika,** Tatizo la ukosefu wa chakula nchini na lishe duni bado linaathiri familia nyingi hasa watoto chini ya umri wa miaka mitano. Kutokana na lishe duni watoto wamekuwa wakiugua utapiamlo na kudumaa (malnutrition and stunt). Kutokana na madhara haya watoto wengi wanaathirika ubongo na kupunguza uwezo wa akili (blunts intellect ), na hata wakifikia umri wa utu uzima huathiri uwezo wao wa kuzalisha na hivyo kuchochea umaskini .

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa tafiti zilizofanywa na Ifakara Health Institute takwimu zinaonyesha kuwa zaidi ya watoto milioni 2.5 katika taifa hili wamedumaa, na vifo vinavyotokana na utapiamlo ni takribani vifo 43, 000 kwa mwaka. Pamoja na hayo watoto wenye utapiamlo uliokithiri ni takribani 430,000 kila mwaka na miongoni mwao walio katika hatari za kufariki endapo hatua za haraka hazijachukuliwa ni takribani watoto 100,000. Kwa idadi hii ya vifo vinavyotokana na utapiamlo takwimu zinaonyesha mtoto 1 hufariki kila baada ya dakika 12.

**Mheshimwa Spika**, Pamoja na hayo, ripoti mbalimbali za afya zimeonyesha Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zenye tatizo kubwa la utapiamlo barani Afrika na duniani kwa ujumla tumefikia kufananishwa na Kongo DRC ilioko katika vita.

**Mheshimiwa spika** Katika ripoti hizo ikiwemo ya Shirika la utafiti la Twaweza zinaonyesha Tanzania ni nchi ya kumi (10 ) duniani kwa ukubwa wa tatizo hili ukilinganisha na nchi kama Ethiopia ikiwa ni ya saba (7) na Sudan Kusini ikiwa ni ya kumi na tano (15) ambapo nchi hizi zimekuwa zikikumbwa na mabaa ya njaa mara kwa mara.Hii ni aibu kubwa kwa ustawi wajamii yetu.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka serikali kutoa tamko ina mkakati gani wa kuhakikisha inatumia mfumo wa kuongeza virutubisho katika kila lishe inayokwenda sokoni ili kuhakikisha wananchi wanakula mlo wenye virutubisho na vilevile kusaidia jamii kutofautisha kati ya **lishe** na **shibe**

## 6.0 RASILIMALI WATU KATIKA SEKTA YA AFYA

**Mheshimiwa Spika,** Kwa takwimu za Wizara ya Afya za mwaka 2014 kuna watumishi wa Afya 15 kwa kila watu 10,000 ilihali Shirika la Kazi Duniani linapendekeza uwepo wa watumishi 41 kwa kila watu 10,000 ili kuweza kutoa huduma bora za Afya kwa kila mwananchi.

Pamoja na Tanzania kuwa ni nchi yenye uhaba mkubwa wa wataalamu wa tiba, wale wachache waliopo wamekuwa wakipata tabu kubwa katika utekelezaji wa majukumu yao, mazingira wanayofanyia kazi ni hatarishi, kuanzia hali ya shughuli zao na hata uduni wa huduma za afya kutokana na ukosefu wa dawa na vifaa tiba na kupelekea lawama nyingi kuelekezwa kwa madaktari na wauguzi hadi kufikia kupigwa na wananchi wanaokosa huduma hizo.

**Mheshimiwa Spika,** sekta ya afya ni sekta ya utoaji wa huduma, hivyo utendaji katika sekta hii kama zilivyo sekta nyingine za utoaji wa huduma zinategemea kwa kiasi kikubwa watendaji wake wana morali ya kazi kwa kiasi gani, na akili ziko katika utulivu kwa kiasi gani. Utoaji wa huduma hutegemea kwa asilimia kubwa aina ya vifaa vilivyopo; morali ya kazi kutokana na jinsi gani watendaji mahitaji yao ya kimsingi yanatatuliwa, ili nao wasiwe katika hali ya kukata tamaa ya maisha na kuwaweka vizuri kiakili ili watoe huduma kwa upendo wenye ari kuu.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kujitafakari upya kuhusu maslahi ya watoa huduma katika sekta nzima ya afya hasa madaktari kwenye ***"call allowance, postmorterm allowance na motisha zingine"*** ili matarajio yao yaweze kufikiwa, ukweli ni kuwa unaweza kuwa na madawa, vifaa tiba na vitendanishi bila watendaji walio na moyo wa kazi hakuna huduma

bora.

### 6.1 Ajira za wataalamu wa Afya

**Mhesimiwa spika** Kambi Rasmi ya Upinzani ingependa kupatiwa sababu za kwa nini wanafunzi waliohitimu mafunzo kwenye sekta ya afya na maendeleo ya jamii hawajapatiwa ajira ilihali kuna upungufu mkubwa wa watumishi hao, hususan katika vituo vipya vilivyojengwa chini ya Mpango wa MMAM na kwa nguvu za wananchi? Inakadiriwa kuwa wataalamu hao wa afya ambao hawajaajiriwa kwa mwaka 2015 ni takribani 1,025 hadi sasa. Tunaitaka serikali kulieleza bunge hili ni hatua zipi za haraka zinachukuliwa kuwaajiri wahitimu hawa na kuziba pengo lililopo baina ya hitaji halisi la watoa huduma na wahitaji wa huduma za afya nchini.

## 7.0 HOSPITALI ZA WILAYA NA HOSPITALI TEULE ZA WILAYA

**Mheshimiwa Spika,** Uendeshaji wa hospitali za wilaya umeendelea kuwa wa kusuasua na mgumu kutokana na Serikali kutotenga fedha za kutosha za maendeleo, vifaa tiba madawa na vitendanishi. Pamoja na baadhi ya hospitali za wilaya kuendelea kuandikia na kutoa taarifa kwa wizara juu ya upungufu huo, hali hii imeendelea kujirudia kila mwaka hali inayosababisha ukwamaji wa shughuli mbalimbali muhimu katika utoaji wa huduma za afya kwa wananchi ambao wengi wana kipato duni.

**Mheshimiwa Spika,** hospitali teule za wilaya ni moja ya wahanga wa tatizo hili, fungu la dawa ni dogo,fungu la pamoja (busket fund )limepunguzwa na fungu la matumizi mengineyo (**OC)** hawapati kabisa , shughuli za msingi kutokana na kupanda kwa gharama za maisha pamoja na idadi ya wagonjwa inayoongezeka kila siku. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutenga fedha za kutosha kutoka fedha za ndani ili kuongeza ufanisi.

### 7.1 Ufanisi katika utendaji wa Hospitali teule

**Mheshimiwa spika** nitolee mfano hospitali ya Selian pamoja na kutoa uduma ya mama na mtoto bure, wazee bure, watu wanoishi na virusi vya ukimwi na saratani bure (cancer)na huduma kwa

watoto yatima zaidi ya 600, upasuaji wa vistulla bure na kuwatembelea nyumbani wagonjwa (home based care).

Baadhi ya huduma hizi hospitali za serikalini hazitoi, ikizingatiwa kuwa bei ya tiba ni sawa, bado huduma hospitali za Dini ni bora kuliko za serikali

**Mheshimiwa Spika,** tunaweza tukafikiri kirahisi kuwa hospitali za dini kuwa zinapata msaada toka nje, lakini tujiulize je kati ya serikali na dini nani mwenye jukwaa bora zaidi la kusema na wahisani? bila shaka ni serikali, hospitali hizo teule pamoja na kutopata ruzuku kama ilivyo kwenye mikataba bado wanatoa huduma bure zilizoko kwenye sera ya umma, cha kushangaza huduma zao ni nzuri kuliko hospitali za serikali, na kulipa watu mishahara mfano hospitali ya Selianin Arusha mishara mil 178 kila mwezi, na milioni 80 ikiwa ruzuku ya serikali, milioni 98 wamekusanya kwenye mapato ya ndani.

**Mhesimiwa Spika**, jambo la kujiuliza ni kwamba hospitali za serikali hawalipi mishahara kutokana na mapato ya ndani mishahara inatoka Serikali, lakini huduma zake bado ziko chini wakati ukilinganisha na hizi teule pamoja majukumu na tozo zina fanana, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuangalia kwa makini tatizo liko wapi na kutafuta tiba ya kudumu ili kuondoa tatizo husika.

## 7.2 Hospitali za Mikoa

**Mheshimiwa spika**, Hospitali za mikoa zina hali isiyoridhisha na huduma zake hazikidhi mahitaji yanayotakiwa kutolewa kama zilivyoitwa hospitali za rufaa za mikoa hali hii inatokana na bajeti ndogo toka serikalini pamoja na mtizamo mbovu wa namna ya uendeshaji,

**Mheshimiwa spika**,Kambi Rasmi ya upinzani ilitembelea hospitali zaidi ya tano za mikoa kupata hali ilivyo ,katika hospitali moja wapo ya mkoa tuliwakuta wakiandaa bajeti yao kulingana kiwango cha fedha walicho agizwa (ukomo wa bajeti) kuwa ndio wanachoweza kupata , kiwango ambacho kilikuwa ni kidogo sana na haitoshi hata kuendesha hospitali kwa kipindi cha miezi sita

**Mheshimiwa spika**, nitolee mfano eneo moja la vitendanishi vya maabara; tulipofanya ziara tulibaini kuwa zipo hospitali walizoomba vitendanishi kwa zaidi ya miezi minne kutoka MSD bila mafanikio, kwa bahati nzuri siku hiyo ndio siku waliyofanikiwa kupata majibu yao toka MSD, baada ya kusubiri kwa miezi minne iliyopita. Katika majibu hayo, walipewa bei ya vitendanishi vya maabara vya matumizi kwa mwezi mmoja tu. Na hii ikiwa ni sehemu tu vitendanishi vyote.Vitendanishi hivi vilikuwa vinagharimu milioni 12.

**Mheshimiwa spika,** zaidi ya yote ni kwamba hospitali hiyo imepewa gawio la milioni 13 kwa mwaka ujao kwa ajili ya vitendanishi, kwa bei hizo za MSD. Hii inamaanisha kuwa hospitali hiyo kwa mwaka ujao itakaa miezi 11 bila vitendanishi vya maabara

**Mheshimiwa Spika** swali, Je, kama maabara haifanyi kazi wananchi watapataje huduma bora ya afya? vipi kuhusu upunguzaji wa vifo vya mama na mtoto? Je, bila maabara hospitali itakuwa hospitali au ni kituo cha kupiga ramli?

### 7.3 Maduka ya dawa kwenye Hospitali za Serikali

**Mheshimiwa Spika,** Maduka ya MSD yalipelekwa karibu na hospitali. Hii siyo tu inapingana na zana nzima ya uchangiaji huduma (cost shairing),lakini jambo kubwa ni kuwa Kambi Rasmi ya Upinzani iliojionea kwenye maduka haya ni kwamba inawapelekea udhibitisho kwa wananchi kuwa imani iliyokuwa imejengeka kuwa madaktari walikuwa wakiiba dawa kwa kiasi kikubwa sio kweli bali serikali ilikuwa haileti dawa. Wananchi sasa wanapata fursa ya kujionea kwa macho yao kuwa MSD hakuna dawa.

**Mheshimiwa Spika,** katika Hospitali mojawapo ambayo ni binafsi iliyotembelewa na Kambi Rasmi ya Upinzani ilikuwa na duka la dawa nje ya hospitali. Dhana nzima ya kuweka duka hili ilikuwa tofauti na vile ilivyoeleweka na MSD. Nia ya MSD ilikuwa ni kuweka dawa, vitendanishi na vifaa tiba ambavyo havipatikani MSD. Lakini duka hilo nilikuwa likifanya biashara ya vitendanishi na vifaa tiba hivyo kama chanzo cha kuongeza mapato ya ndani katika kuendesha hospitali hiyo.

Kambi rasmi ya Upinzani ,inaishauri serikali ijifunze kutoka sekta binafsi jinsi ya kuweza kuendesha maduka ya dawa ambayo wameyaanzisha kwenye hospitali zetu.

## *8.0 MAMLAKA YA CHAKULA NA DAWA-* **TFDA**

**Mheshimiwa Spika**,Serikali ina Mamlaka ya chakula na dawa nchini (TFDA) ambayo ina jukumu la kukagua vyakula, madawa na vipodozi vinavyoingia nchini ,Pamoja na mamlaka hizi kuna mamlaka lukuki zinazohusika na ukaguzi wa bidhaa hizi, kuanzia zinapoingia nchini mpaka zinapomfikia mlaji

**Mheshimiwa Spika**, Matumizi ya madawa na vipodozi yamekuwa mzigo mkubwa kwa vijana hususani vijana wa kike. Katika ripoti iliyoandika na YWCA "Beauty at any cost"Ulibaini kuwa wanawake wanatumia fedha nyingi katika kubadilisha muonekano wa maumbile yao.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na hayo athari za madawa na vipodozi haramu kiafya ni kubwa kwani imechangia ongezeko la magonjwa ya saratani ya ngozi, via vya uzazi, na hata madhara makubwa kwenye viungo vingine vya mwili.

**Mheshimiwa Spika,** Bila shaka madawa na vipodozi hivi haramu nchini vinapita katika viwanja vya ndege, bahari na hata mipakani kwa njia ya barabara Lakini Pengine rushwa na uzembe vinaweza kuwa chanzo cha ukiukwaji wa taratibu za ukaguzi.

**Mheshimiwa Spika** hapo juu umeona gharama kubwa inayotumika kuagiza na kusafirisha madawa, vitendanishi na vifaa tiba toka nje ya nchi kupitia bandarini, Kambi Rasmi ya Upinzani wakati wa ziara yake Ilibaini kuna baadhi ya madawa na vifaa tiba ambayo havipatikani nchini lakini vinapatikana katika nchi za Afrika Mashariki ,lakini hizo dawa hazija sajiliwa nchini na TFDA kutokana na urasimu .

**Mheshimiwa Spika** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali ijiridhishe kwanini tuagize kutoka India wakati vitu hivi vinapatikana Africa Mashariki? Pili, serikali ijiulize kama tunaagiza madawa yanayopatikana Afrika Mashariki kutoka nchini India Je, tunazingatia

vigezo gani ?

## 9.0 HUDUMA ZA AFYA KWA WATOTO WAISHIO KATIKA MAZINGIRA HATARISHI

**Mheshimiwa Spika,** Suala la Afya ni suala muhimu kwa kila binadamu, afya haichagui rangi, kabila, dini, umri, jinsia wala mazingira anayotoka mtu. ***(Health is vitally important for any human being, whatever our differences maybe, health is our most important commodity.***

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania ni moja ya nchi iliyoridhia Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watoto "Convention on the Right of a Child" (CRC). Mkataba huo umeelezea bayana katika kifungu cha 24 kuwa nchi washiriki watahakikisha hakuna mtoto atakae kosa haki yake ya kupata huduma ya afya ***"They shall strive to ensure that no child is deprived of his or her right of access to such health care services"***

***Mheshimiwa Spika,*** Kwa mujibu wa Sheria ya Haki ya Mtoto ya mwaka 2009 (Law of the Child Act), inatambua haki ya kila mtoto kupata huduma bora ya afya bila ubaguzi. Lakini haki hii imekuwa ikikiukwa au kuporwa hasa kwa watoto waishio maeneo hatarishi. Katika takwimu mbalimbali zilizotolewa na mashirika yanayotoa huduma kwa watoto waishio mitaani imeonyesha kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa sana la watoto waishio mitaani. Hii ni kutokana na changamoto mbalimbali za kimaendeleo, mifumo wa kiuchumi, mabadiliko ya malezi na makuzi, n.k Ni vyema serikali ikatambua wapo watoto waliozaliwa na kukulia mitaani kinyume na mapenzi yao .Watoto hawa hawafahamu ndugu wala jamaa zao zaidi ya wale wanaoishi nao huko mitaani. Watoto hawa hawapati huduma yoyote ya msingi ikiwemo huduma za afya. Hata pale anapougua akiwa mtaani imekuwa ni vigumu sana kwenda zahanati kupata huduma ya afya. Hii ni kwa sababu watoa huduma hizi hawatengenezi mazingira rafiki ya kuwahudumia watoto hao, changamoto ya kukosa fedha kwa ajili ya matibabu na dawa, na zaidi ni kukosa uelewa kuhusu maswala ya afya.

***Mheshimiwa Spika,*** pengine serikali haijaona moja kwa moja

madhara haya makubwa kwa watoto na vijana waishio mitaani kukosa elimu ya afya na huduma za afya. Endapo hali hii ya kuwanyima watoto wa mitaani haki ya kupata huduma ya afya na elimu juu ya masuala ya afya ni dhahiri watoto hawa watakuwa katika hatari ya kupata maambukizi ya magonjwa na hata kuambukiza wengine na jamii kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** Watoto hawa waishio mitaani wengi husumbuliwa na magonjwa mbalimbali, yakiwepo magonjwa ya zinaa (sexually transimited diseases) ikiwemo UKIMWI.Vilevile, kwa kukosa elimu ya afya wengi hawatambui madhara ya matumizi ya dawa za kulevya, dalili za magonjwa na namna ya kujikinga na magonjwa. Kutokana na mazingira watoto hawa wanapoishi wako katika hatari kubwa ya kupata magonjwa ya milipuko kama kuhara na kipindupindu na hivyo kuiweka jamii nzima katika hatari ya maambukizi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuhakikisha kuwa katika makundi maaalum ya wanaofaidika na huduma ya afya bila malipo nchini katika hospitali za serikali ikiwemo wazee, watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano na kina mama wajawazito basi watoto wainaoishi mitaani wawe kati ya kundi litakalopata huduma ya afya bila malipo (exemption).Kuonyesha upendo kwa watoto hawa ni njia kuweza kufungua milango ya mazungumzo ili kutafuta mbinu ya kuwaondoa mitaani au kupunguza ongezeko .

## 10.0 MAENDELEO YA JAMII

**Mheshimiwa Spika,** ni ukweli tupo hapa tulipo kwa ajili ya kutokujali au kutokutilia mkazo kazi zinazofanywa na wataalam wa maendeleo ya Jamii. Taaluma hii ndiyo inayohusika kwa kiasi kikubwa kuielimisha jamii juu ya maadili, na sasa hivi kama taifa tunatatizo kubwa sana la maadili. Tasnia hii ikitumika na kupewa umuhimu unaostahili tutaboresha **"maadili kwa Taifa"**.

## 10.1 Maendeleo ya Wazee Nchini

**Mheshimiwa Spika,** wazee ni hazina ya taifa. Na kwa mujibu wa sensa ya makazi na watu ya mwaka 2012, idadi ya wazee nchini ni milioni 4.15 sawa na asilimia 9.5 ya idadi ya watu wa Tanzania bara pekee ambapo kati yao, wanawake ni milioni 2.18 na wanaume ni milioni 1.97. Wazee wa taifa hili wanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo umaskini uliokithiri, mauaji dhidi ya vikongwe, ubakaji, ukosefu wa huduma za afya, upungufu wa chakula, kukosekana kwa makazi ya wazee na kadhalika. Hali halisi ni kwamba wazee wengi wamejiajiri katika sekta isiyo rasmi na wengi wanajishughulisha hasa na kilimo duni na wengine wana majukumu ya kulea familia zao duni.

**Mheshimiwa Spika** kuna tatizo kubwa katika utoaji wa huduma za afya kwa kundi hili la wazee ambapo pamoja na Serikali kutoa maamuzi ya kutoa huduma za afya bila malipo kwa wazee mwaka 2007, agizo kwa halmashauri kutenga dirisha maalum kwa ajili ya huduma kwa wazee bado kuna ombwe kubwa katika utoaji na upatikanaji wa huduma za afya kwao. Leo hii, wazee wengi wanapata matibabu duni kwenye hospitali hizo ambapo mzee anamuona daktari tu bure lakini hapati dawa wala huduma nyengine hazipatikani kwa bure kama inavyotakiwa.

Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni inataka kujua, pamoja na halmashauri kuagizwa kutenga dirisha maalum la kuhudumia wazee, je ni halmashauri ngapi mpaka sasa zimetenga madirisha hayo na halmashauri ngapi zimechukuliwa hatua kwa kushindwa kutekeleza agizo hilo? Ni lini Serikali itagharamia matibabu kwa wazee kwa kupitia mfumo wa bima ya afya?

## 10.2 VYUO VYA MAENDELEO YA JAMII NA WANANCHI

**Mheshimiwa Spika,** kwa muda mrefu sasa kumekuwa na changamoto za kiutendaji ikiwemo miundombinu mibovu, mazingira duni na uchakavu wa majengo hali inayopelekea kuwa na mazingira magumu ya kujifunzia na kufundisha. Katika bajeti ya mwaka 2015/2016 vyuo vya maendeleo ya jamii vilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 2 fedha za ndani lakini mpaka Machi, hakuna

fedha zilizotolewa.

Aidha, Taasisi ya maendeleo ya jamii ya Tengeru ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 1kwa ajili ya ujenzi wa maktaba nayo pia haikupata hata shilingi moja ya fedha zilizotengwa. Pamoja na Serikali kueleza kuwa udahili wa wanafunzi katika vyuo hivyi umeongezeka, kuna hatari kubwa ya vyuo hivyi kufungwa kutokana na uchakavu mkubwa wa majengo na uwezo duni wa kuweza kutoa elimu kwa wadahiliwa na hata kuzalisha wahitimu hewa wasio na elimu bora kutokana na uhaba wa vifaa vya kufundisha.

### 10.3 Uhitaji wa Maafisa Maendeleo ya Jamii Nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kuendelea kuporomoka kwa maadili nchini kwa kiwango kikubwa kunachangiwa na uhitaji mkubwa wa maafisa maendeleo ya jamii. Hata hivyo, katika halmashauri 180 nchini (Tanzania Bara) kuna uhaba wa takribani asilimia 66.3 wa maafisa maendeleo ya jamii kwani katika kata 3957, kuna upungufu wa maafisa maendeleo ya jamii 2625 . Je kwa hali hii mmomonyoko wa maadili unaweza kuepukika?

## 11.0 BENKI YA WANAWAKE TANZANIA

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012 inaonesha kuwa wanawake nchini Tanzania ni asilimia 51 ya watanzania wote. Kwa mwaka 2015/16 inaonesha kuwa jumla ya shilingi 20,124,874,328 zilikopeshwa ambapo wanawake walipata mikopo nyenye thamani ya shilingi 12,878,977,228

**Mheshimiwa Spika**, hii inaonyesha kuwa bado serikali haijaonyesha nia ya dhati ya kuwasaidia wanawake kupitia benki hii. Mpaka sasa kati ya mikoa 30 ni mikoa 7 tu ndio wanaonufaika na mikopo kupitia benki hii ya wanawake.Kati ya mikoa hiyo ni mikoa ya Dar es Salaam,Dodoma,Mwanza,Mbeya,Iringa,Ruvuma na Njombe na hakuna mkoa wowote kutoka Kanda ya Kaskazini.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na hayo bado riba inayotozwa na benki

hii ni kubwa sana.Tofauti na benki nyingine nchini zenye riba nafuu, benki hii ya wanawake inatoza riba ya asilimia 19. Huku ni kuongeza umaskini kwa mwanamke wa Tanzania na sio kumkomboa kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua ni lini serikali itahakikisha kuwa Benki hii inapunguza riba ili kuwanufaisha wanawake wajasiriamali? Vilevile serikali ituambie mkakati wake wa kuhakikisha inapanua wigo wa kutoa huduma nchini ili kuhakikisha wanawake nchi nzima wananufaika?

### 11.1 Kuzuia Ukatili wa Kijinsia

**Mheshimiwa Spika**, Bado tatizo la ukatili wa kijinsia nchini ni kubwa sana. Matukio yanayotokana na ubakaji, ulawiti, vipigo kwa wanawake, tohara kwa wanawake na watoto wa kike, ndoa na mimba za utoto bado vinaripotiwa katika vyombo mbalimbali vya habari japo matukio mengi pia yanashindwa kuripotiwa kutokana na changamoto mbalimbali za kimawasiliano.

**Mheshimiwa Spika,** vitendo hivi vinadhalilisha utu wa mwanamke na ni kinyume cha Azimio la Beijing la mwaka 1995 ambapo nchi yetu ni miongoni mwa nchi zilizoridhia azimio hilo. Kuendelea kushamiri kwa vitendo hivi hususani maeneo ya vijijini kunaonyesha uhitaji mkubwa wa kuanzisha Dawati la Jinsia mpaka ngazi ya vijiji kwa vitendo na sio kinadharia kama ilivyo sasa.

**Mheshimiwa Spika,** Je, serikali imetenga kiasi gani cha fedha katika bajeti yake ili kuhakikisha kuwa kila kijiji kinakuwa na Dawati la Jinsia hii ikiwa ni pamoja na kuwaajiri watumishi wa dawati la Jinsia?

### 11.2 Huduma za Sheria

**Mheshimiwa Spika**, "***injustice anywhere is a threat to justice everywhere" Udhalimu mahali popote ni tishio la haki kila mahali"*** Bado kuna manyanyaso, ukatili na hakuna haki kwa watoto wengi walioko magerezani au wale wenye kesi. Watoto hawa wananyimwa haki kuanzia kwenye usikilizwaji wa kesi zao mpaka kwenye mazingira wanayoishi ndani ya magereza. Katika Randama ya taarifa ya Utekelezaji ya mwaka 2015/2016 taarifa ya hali za magereza nchini ilikiri kuwa haki za watoto katika mahakama zetu

zinakiukwa sana. Watoto wadogo wanachanganywa na watu wazima, wenye tabia tofauti, wenye kesi zinazohatarisha hata usalama wa watoto hao ndani ya magereza. Wapo wenye kesi za kulawiti na kubaka, majambazi sugu n.k wote hawa wanachanganywa na watoto hao. Hii yote ni ukiukwaji mkubwa wa haki za watoto na udhalilishaji wa utu wa watoto hao.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hayo, huduma za msaada wa kisheria kwa watoto hawa imekuwa ni changamoto kubwa kwa kuwa mawakili wanaojitokeza kuwasaidia ni wachache au mashirika yanayotoa huduma ya msaada wa kisheria yamezidiwa na wingi wa kesi. Pia watoto hawa wanatoka katika familia duni, na kesi zao zinachukua muda mrefu. Katika Randama ya taarifa ya utekelezaji ni watoto 25 tu waliopata msaada wa kisheria na watoto 16 tu ndio waliopata uwakilishi mahakamani. Serikali haitendi haki kwa watoto hawa hata kidogo nani ukiukwaji wa  Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watoto (Convention on the Right of the Child).

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuhakikisha kuwa watoto ho wanaochanganywa na watu wazima wanatengwa mara moja ili kulinda haki na utu wao kama watoto.

Serikali ituambie ina mpango gani wa kuanza kutumia paralegals ili kuweza kuwasaidia watoto hao kupata haki zao kama ilivyofanikisha kutumia para social workers katika maeneo mbalimbali nchini?

**Mheshimiwa Spika**, SHUJAA NI MTU YULE ANAEMJALI MTOTO WA KIKE MIMI NI SHUJAA, JE WEWE?

Naomba kuwasilisha,

**DR GODWIN OLOYCE MOLLEL (MB)**

Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi-Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia wazee na Watoto.

**11.05.2016**